

WIZARA YA KILIMO



BODI YA KOROSHO TANZANIA



MWONGOZO WA UNUNUZI, USAMBAZAJI, NA UUZAJI WA PEMBEJEO ZA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2018/2019

*Umeandaliwa na:
Bodi ya Korosho Tanzania,
S. L. P 533,
Mtwara.*

JUNI, 2018

SEHEMU YA KWANZA

MWONGOZO WA UNUNUZI, USAMBAZAJI NA UUZAJI WA PEMBEJEU ZA ZAO LA KOROSHO MSIMU WA 2018/2019

1.0 UTANGULIZI

Katika msimu wa 2018/2019, Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania inasimamia ununuzi na uuzaji wa viutilifu vya zao la korosho kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja yaani “Bulk Purchase”.

Mfumo huu unahakikisha kuwa pembejeu za zao la korosho kwa mkulima zinapatikana kwa wakati, kwa bei nafuu na kwa urahisi. Katika kutekeleza azma hii, Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma huzingatiwa kwa kupitia utaratibu wa kutangaza zabuni. Zoezi hili husimamiwa na Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na wadau mbalimbali.

Wadau mbalimbali wanahusika kwa namna moja au nyingine katika shughuli ya ununuzi, usambazaji na uuzaji wa pembejeu za zao la korosho. Hivyo, mwongozo huu unatoa utaratibu mzima wa ununuzi na uuzaji wa pembejeu hizo. Aidha, mwongozo unaainisha majukumu ya kila mdau husika katika kuhakikisha pembejeu zinawafikia wakulima kwa wakati na kiasi kilichopangwa.

2.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu unatoa maelezo na maelekezo ya kina kuhusu ununuzi, ugawaji na usambazaji wa pembejeu za salfa ya unga na viutilifu vya maji. Jumla ya vituo 18 vimetengwa na Bodi ili kumrahisishia mkulima kupata pembejeu hizi. Aidha, Mwongozo huu unaainisha majukumu ya kila Mdau husika katika kuhakikisha viutilifu vinawafikia wakulima kwa wakati, kwa bei nafuu na kwa urahisi zaidi. Jukumu la kila Mdau ni kutimiza wajibu wake katika kufanikisha zoezi la usimamizi wa pembejeu hizi.

